ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe.Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais

25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani

45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Thalathini na Nne – Tarehe 31 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

KUAHIRISHWA BARAZA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuita na kumuomba mHe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya hotuba ya kuahirisha mkutano huu, naomba nichukue nafasi tena kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kazi nzuri sana ambayo tumeifanya tangu tarehe 15 Juni, 2011 hadi leo hii kumalizia kwa ajili ya kuahirisha mkutano wetu huu.

Lakini naomba pia niwashukuru watendaji wote serikalini ambao wamewasaidia Waheshimiwa Mawaziri kufanya shughuli zao za hotuba mbali mbali kwa ufanisi na hatumaye kutoa majumuisho katika Baraza hili, ambayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa ni mazuri na yalifanikisha shughuli zetu.

Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi kubwa na nzuri mliyoifanya kufanikisha shughuli zetu. Lakini shughuli zetu hizi kama nyinyi hamkunisaidia nyinyi nisingeweza kuzifanya. Pia mimi vile vile nimesaidiwa kwa dhati kabisa na Mhe. Naibu Spika, amenisaidia sana katika shughuli hizi wakati wowote niliokuwa nina dharura basi nikimpigia simu tu ananambia timamu nakwenda, afande nitafanya kazi. Japo sikuwa mwanajeshi lakini alikuwa ananiita afande wakati mwengine.

Wakati huo huo wenzetu Wenyeviti Mhe, Mahmoud Mohamed Mussa na Mhe. Mgeni Hassan Juma nao wamesaidia sana katika kufanikisha kuongoza shughuli za mkutano huu wote. Wote nawashukuru sana kwa dhati na kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kwa pamoja kwa mashirikiano makubwa.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wake wote nawashukuru kwa kazi nzuri waliyoifanya. Shughuli hizi zote zimekwenda vyema kwa sababu ya mashirikiano ya pamoja. Niiombe serikali basi mashirikiano haya ya pamoja ndio changamoto iliyoko mbele yetu ili kama tulivyosoma dua hapa tuweze kushinda matatizo yetu ambayo yapo katika shughuli zetu za serikali. Sasa Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika,Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Waandishi wa Habari Mabibi na Mabwana Assallam Aleykum.

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kumaliza salama na kwa mafanikio makubwa Mkutano wa Nne wa Bajeti ya Mwaka 2011/2012. Huu ni Mkutano wa Kwanza wa kihistoria wa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni Serikali yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Katika muda wote tuliokuwa hapa tumeonesha mshikamano wa hali ya juu kabisa wakati tukijadili na kupitisha Bajeti ya Serikali na Bajeti za Wizara mbali mbali. Ni vyema mshikamano huu tuliouonesha tukiwa Barazani wakati wa kujadili na kupitisha Bajeti za Wizara zetu tuendelee nao na wakati wa utekelezaji wa bajeti hizo.

Mhe. Spika, leo sikusudii kutoa hotuba refu, kwani tayari tumeshasikiliza hotuba nyingi za Bajeti ya Serikali na hotuba za wizara mbali mbali, nyengine zikiwa refu kama Hotuba ya Bajeti ya Serikali, Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yangu. Hivyo, nitakachokifanya leo hii ni kueleza machache ya kutoa shukrani na kusisitiza baadhi ya mambo muhimu yaliyojitokeza katika mijadala yetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi, Naibu wako wa Spika na Wenyeviti wako kwa namna mlivyoliongoza Baraza letu tukufu hadi kumalizika kwa mkutano huu kwa salama na mafanikio makubwa. Busara na hekima zako zimesaidia kufanikisha kwa kiwango cha juu kuendesha mijadala katika kikao hiki cha Bajeti ya mwaka 2011/2012 kilichoanza tarehe 15 Juni, 2011 na kumalizika leo tarehe 31 Julai, 2011.

Mhe. Spika, vile vile, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha Bajeti za Wizara zao kwa ufanisi pamoja na kujibu hoja na maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa umakini na usahihi wa hali ya juu.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa namna walivyotumia haki yao kama Wawakilishi wanaowatumikia wananchi, kuchangia hotuba mbali mbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri mbali mbali, tukianzia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali pamoja na hotuba za Mawaziri wengine. Waheshimiwa Wajumbe walizisikiliza hotuba hizo kwa makini, kuzichangia kwa dhati, walitoa maoni yao kwa ukweli na uwazi. Kwa kweli Wajumbe waliwatikisa Mawaziri na kuwafanya wawe macho zaidi.

Kwa msemo wa Kingereza “Mawaziri *were kept on their toes*”. Buti zilikuwa nyingi kwa msemo wenu wenyewe kwa baadhi ya wizara. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kututanabahisha mambo mengi ambayo yametupa serikali faida kubwa ya kutuwezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba yale yote ambayo serikali imeahidi kuyatekeleza nitahakikisha kuwa mambo hayo yanatekelezwa ipasavyo.

Mhe. Spika, jambo la kufurahisha zaidi ni kwamba pamoja na buti nyingi ambazo baadhi ya wizara zilipata, lakini hatimaye Waheshimiwa Wajumbe wako waliweza kuzipitisha bajeti hizo kwa kauli moja.

Mhe. Spika, kwa aina ya pekee, naomba kutoa pongezi za dhati kwa ndugu yangu Mhe. Ali Mzee Ali kwa kuteuliwa tena na Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Mjumbe wa Baraza lako tukufu. Hii inaonyesha imani kubwa ya Mhe. Rais wetu mpendwa aliyonayo juu yake kutokana na uwezo na uzoefu wake katika Baraza hili. Tunaamini Mhe. Ali Mzee Ali ataendelea kutoa michango yake mizuri kwa Baraza kama ilivyo kawaida yake, kwani baadhi yetu ambao hatukuwemo katika Baraza lililopita ambapo Mhe. Ali Mzee alikuwa Mwenyekiti, tutafaidika sana kutokana na uwezo na uzoefu wake huo.

Mhe. Spika, pia nawashukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim pamoja na watendaji wake wote wa Baraza kwa kazi nzuri waliyofanya kufanikisha kufanyika kwa kikao hiki cha Bajeti kwa mafanikio. Nawashukuru kwa uvumilivu wao, na hasa ile sehemu ya Uhasibu ambayo ilituhudimia vyema. Halikadhalika, nawashukuru kwa dhati ndugu zangu Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwafikishia wananchi wetu hotuba za bajeti zilizowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na majadiliano katika Baraza hili. Kupitia kwao wananchi walikuwa wakifuatilia kwa karibu zaidi kila tulichozungumza hapa Barazani. Ahadi tulizozitoa wanazijua; mipango tuliyoipanga wanaifahamu na habari zote hizi zimewafikia wananchi kupitia vyombo vyetu vya habari.

Shukrani maalum nazitoa kwa TVZ na Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa mpango wao mzuri uliowezesha wananchi wetu kuona na kusikia moja kwa moja maendeleo na shughuli za Baraza za kila siku. Haya yalikuwa mafanikio makubwa kwa vyombo vyetu vya habari. Nawapongeza sana.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kufuatilia kwa karibu zaidi mijadala iliyokuwa ikiendelea hapa Barazani. Ni matumaini yangu kuwa sasa wanasubiri kwa hamu utekelezaji wa

mipango ya maendeleo tuliyowaelezea hapa Barazani. Wananchi wamejenga matumaini makubwa kwa Serikali yao ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Kwa maana hiyo, naamini sote tunaondoka hapa tukiwa kitu kimoja katika kuwatumikia wananchi wetu. Nimeambiwa kuwa Baraza hili limekuwa tofauti na Mabaraza mengine yaliyopita. Baraza hili wanasema lilikuwa kiboko.

KUIMARIKA KWA DEMOKRASIA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI:

Mhe. Spika, katika mkutano huu Waheshimiwa Wajumbe wameweza kutumia demokrasia yao kuihoji serikali na wameonyesha ukomavu wa kisiasa katika kuchangia Bajeti ya Serikali bila ya kujali itikadi zao na vyama vyao. Hali hii, inaonyesha dhamira ya kuimarisha umoja miongoni mwa Wajumbe na hilo ndio lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile, hali hii imewapa wananchi matumaini makubwa kwamba Waheshimiwa Wajumbe wapo kitu kimoja katika kutetea maslahi ya wananchi na taifa.

Mhe. Spika, baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako walionyesha mashaka makubwa kwa baadhi ya mambo yaliyofanyika Serikalini kwamba yalifanyika bila ya kufuata utaratibu. Ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba Serikali ya Awamu ya Saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa, ikiongozwa na Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, Rais wetu mpendwa haitavumilia hata kidogo uchafu wa aina yoyote wa uvunjaji wa sheria na taratibu zilizowekwa, na ndiyo maana nikaliruhusu Baraza lako kuunda Kamati Teule kuchunguza yale mambo ambayo walikuwa na mashaka nayo ili wajiridhishe, na sitosita kuruhusu kuundwa kwa Kamati hizo kila nitakapohisi ipo haja ya kufanya hivyo. Ningependa kuwasihi Waheshimiwe Mawaziri kuzisimamia Wizara zao vizuri ili vitendo hivi vya uvunjaji wa sheria na taratibu visitokee.

MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR:

Mhe. Spika, Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar unatokana na Waasisi wa Taifa letu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Mzee Abeid Amani Karume, ambao walifanya maamuzi kwa niaba ya wananchi na kutokana na dhamira hiyo njema ikatayarishwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa mfumo uliopo ni wa Serikali mbili, mfumo ambao upo Kikatiba. Mfumo huu pia ndio uliokubaliwa hadi sasa na Chama cha Mapinduzi ambacho sera zake ndizo tulizokubaliana kikatiba zifuatwe katika kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ni matumaini yangu kwamba sote tutaufuata muundo huu hadi hapo uamuzi mwengine utakapotolewa.

Mhe. Spika, umetokea mtindo katika siku za hivi karibuni na hasa sehemu za mashamba kwa baadhi ya Wazanzibari kuwafukuza Wazanzibari na Watanzania wenzao katika maeneo yao wanayoishi. Siyo jambo jema Mzanzibari kwa mujibu wa Katiba anayo haki ya kuishi mahala popote mradi havunji sheri. Na Mtanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo haki ya kuishi mahala popote nchini Tanzania bila ya kubughudhiwa mradi havunji sheria. Vitendo vya aina hii vya ubaguzi viachwe mara moja.

KERO ZA MUUNGANO:

Mhe. Spika, Muungano wetu unazo changamoto ambazo Serikali zetu mbili zimejipanga kuzipatia ufumbuzi. Zipo kero ambazo tayari hivi sasa zimeshapatiwa ufumbuzi na bado zipo kero ambazo zinaendelea kuwapatia usumbufu mkubwa wananchi wetu na hivyo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka. Dhamira yetu kama Serikali ni kutekeleza yale yote ambayo yameamuliwa katika Kamati yetu ya pamoja ya kutatua kero za Muungano, na kutokana na dhamira hiyo ndio maana Serikali zetu mbili zimefanya uwamuzi wa kuandaa Mswada wa Sheria wa Kuunda Tume itakayoratibu ukusanyaji wa maoni ya wananchi ambayo yatapelekea kupata Katiba mpya. Naamini wananchi watatumia fursa hii kutoa michango mizuri ambayo itasaidia kuondoa matatizo yaliyopo na kujenga Muungano imara wenye maslahi kwa pande zote mbili za Muungano wetu.

Mhe. Spika, hoja ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia imezungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe. Kama nilivyosema katika majumuisho ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yangu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekubaliana na matakwa ya Waheshimiwa Wawakilishi kwamba suala hili liondolewe katika orodha ya mambo ya Muungano. Bado Serikali zetu mbili zinaendelea kulifanyia kazi suala hili na ni imani yangu kwamba litapatiwa ufumbuzi muafaka. Hivyo, nawaomba tena Waheshimiwa Wajumbe waendelee kuwa na subra na kuamini kwamba busara itatumika katika kulipatia ufumbuzi suala hili kwa maslahi ya Zanzibar na watu wetu.

MAREKEBISHO YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:

Mhe. Spika, kuhusu suala la Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kama ambavyo Serikali imekuwa ikitoa ufafanuzi katika Baraza lako hili Tukufu. Mhe. Spika, kilichojadiliwa mpaka hivi sasa ni Mswaada wa Sheria ya Kuunda Tume ya Kukusanya Maoni ya Wananchi kuhusu kuandaa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mijadala mbali mbali iliyofanyika, ilionekana kuna mapungufu mengi kama ambavyo wananchi wengi wa Tanzania Bara na Zanzibar walivyoainisha. Kutokana na mapungufu hayo, Serikali zote mbili ziliwaagiza Wanasheria Wakuu wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kukaa pamoja na kuyashughulikia yale yote ambayo yalielezwa na kutolewa maoni na Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla. Kazi hiyo ilifanywa kwa pamoja na kwa uwazi na kwamba mswaada wa hivi sasa umezingatia maoni yote yaliyotolewa na Wazanzibari, ingawa bado ipo sehemu ndogo ya kuirekebisha ambayo inafanyiwa kazi na pande zetu mbili.

MAGEUZI KATIKA SEKTA YA SHERIA:

Mhe. Spika, Serikali katika mwaka huu wa fedha kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeazimia kuanza kutayarisha Programu ya Mageuzi katika Sekta ya Sheria *(Legal Sector Reform Program).* Katika hatua ya kwanza ya program hiyo, Wizara itatayarisha mkakati wa mageuzi hayo yaani *(Legal Sector Reform Strategy)* na kufuatiliwa na hatua ya pili ambayo itahusu utekelezaji wa mageuzi yenyewe. Mageuzi haya makubwa yatahusisha taasisi zote za Serikali na zisizo za Serikali zinazohusika na utekelezaji wa sheria na kusimamia utawala wa sheria kwa ujumla. Utekelezaji wa mageuzi haya ni muhimu sana kwani utachangia kupatikana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mageuzi mengine ya kisekta yanayoendelea nchini hivi sasa. Lengo kubwa la mageuzi haya ni kuzijengea uwezo wa kitaasisi *(institutional capacity)* taasisi zote ili kuhakikisha kuwa utawala wa sheria unaimarika hapa nchini. Pamoja na juhudi hizi za Serikali, wadau wa maendeleo nao pia wameonesha nia ya kutuunga mkono katika kutimiza azma yetu hii.

Mhe. Spika, Serikali imesikia vilio vya wananchi kupitia kwa Wawakilishi wao juu ya huduma zisizoridhisha zinazotolewa na baadhi ya Taasisi zake zikiwemo za Usajili wa Vizazi na Vifo na Ndoa na Talaka. Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, hivi sasa imo katika mchakato mkubwa wa kuufanyia mapitio mfumo mzima wa usajili wa vizazi na vifo na ndoa na talaka. Mapitio hayo yatajumuisha utengenezaji wa sheria mpya ya vizazi, vifo, ndoa na talaka; utengezaji wa mfumo wa kisasa wa usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka; na kuunganishwa mfumo huu pamoja na mifumo mingine ya utoaji wa huduma kama ule wa vitambulisho, uhamiaji, upigaji kura na huduma za afya. Yote haya yanalenga kumuwezesha mwananchi kupata huduma hizi kwa haraka na wepesi zaidi.

KUENDELEZA ZAO LA KARAFUU:

Mhe. Spika, kama tujuavyo kwamba hivi sasa Serikali kwa nia njema kabisa imepandisha bei ya karafuu nchini. Uamuzi huu una lengo la kuwawezesha wakulima kumudu gharama za uzalishaji wa zao hili, kupunguza magendo na pia kuhamasisha ukulima wa zao hilo. Hata hivyo, uamuzi huu unachochea changamoto kadhaa zikiwemo wizi wa karafuu zenyewe na hata uharibifu wa miti kwa kukata matawi yenye karafuu na kuondoka nayo. Katika hili, juhudi za pamoja na za makusudi zinapaswa kuchukuliwa kunusuru hali hiyo, kinyume

chake lengo lililokusudiwa halitafikiwa. Hatua za ulinzi lazima zianzie katika maeneo yetu kwa kuimarisha harakati za ulinzi shirikishi. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinatakiwa kuwa imara kwa kuweka mikakati ya kuwadhibiti wahalifu wa nchi kavu na wale wanaosafirisha karafuu nje ya nchi kimagendo. Aidha, vyombo vyetu vinavyosimamia sheria zikiwemo Mahakama navyo viweze kulipa uzito unaostahiki suala hili kwa kuhakikisha kwamba washtakiwa wanaotiwa hatiani kwa makosa kama hayo wanapewa adhabu inayostahiki na itakayotoa funzo kwa wengine. Vitendo hivi vinavyofanywa na baadhi yetu vitadhoofisha sana uchumi wa nchi yetu. Watu hawa ni sawa na wahujumu uchumi. Jambo linalotusikitisha sana ni kwamba baadhi ya Viongozi nao wanahusika na kadhia hii. Tunawaambia kwamba tunaowajua hatutowavumilia. Tusiowajua tutawasaka kwa nguvu zetu zote.

MIGOGORO YA ARDHI:

Mhe. Spika, tumekubaliana kujenga nyumba ya umoja, msingi wake Katiba, kuta zake Utawala Bora, paa lake uwajibikaji, rangi yake si kijani wala buluu lakini inapendeza, madirisha yake haki kwa wote, na milango yake amani na utulivu. Tunajenga nyumba hii kwa njia ya kujitolea na si muda mrefu aliejitolea na asiejitolea tutaishi humo. Lakini, shaka yangu kubwa, na pengine na wenzangu pia iko kwenye vishindo vyetu kwani nyumba hii ni mpya, haiwezi kuhimili vishindo vya watu wengi, na hasa watu wenyewe wakiwa wameshiba! Tusipokuwa waangalifu nyufa ninazoziona kwa mbali hivi huenda zikaishia kuwa mipasuko mikubwa itakayopelekea kuporomoka kwa nyumba yetu.

Mhe. Spika, nyufa hizi ninazoziona si nyengine bali ni migogoro ya ardhi iliyosambaa Unguja na Pemba, Mijini na Vijijini. Migogoro ya ardhi kama ingekuwa nyimbo ya taarab, basi tungesema imepanda chati hapa kwetu. Migogoro hii inatishia utulivu wetu wa kijamii na kisiasa na tusipokuwa waangalifu si leo, wala si kesho, wananchi wetu watakosa imani kwa viongozi wao ambao ni sisi; wananchi wetu watakosa imani na Serikali ambayo tunaingoza sisi.

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Saba chini ya Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein tangu kuingia madarakani imekuwa ikiendeleza juhudi za kutatua migogoro ya ardhi kwa lengo la kuleta utulivu ndani ya jamii yetu lakini pia kwa lengo la kuleta haki, na ndio dhamira ya Mapinduzi yetu.

Migogoro ya ardhi nchini mwetu imejitokeza katika hali ifuatayo: wapo wananchi wanaogombea ardhi waliyorithi; ipo ardhi inayogombewa kwa sababu imeuzwa zaidi ya mara moja; ipo ardhi ya Serikali ambayo imevamiwa; ipo migogoro ya ardhi ambayo wananchi wanyonge wameporwa na vigogo; ipo migogoro ya ardhi ambayo wananchi wameuza kwa bei ndogo kwa wawekezaji na sasa wanadai kulipwa tena bei kubwa baada ya kubaini ardhi imepanda thamani.

Migogoro ya ardhi tayari Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein ameshalitolea maelekezo. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali haitolifumbia macho suala hili na itachukua kila hatua kuhakikisha kwamba matatizo ya migogoro ya ardhi yanapatiwa ufumbuzi ili haki itendeke na kuwa na matumizi mazuri ya ardhi. Napenda kutoa wito tena kwa Viongozi na wananchi kwa jumla kutoendelea kujiingiza katika matatizo ya ardhi na mtu yeyote atakaekwenda kinyume na sheria na taratibu zilizowekwa hazitovumiliwa. Naiomba sana Mahakama ya Ardhi kuharakisha kutoa haki kwa kesi za ardhi zinazopelekwa mbele yake kwa haraka iwezekanavyo.

UTENDAJI WA BARAZA LA MANISPAA:

Mhe. Spika, kama sote tulivyoshuhudia katika mijadala wakati ilipowasilishwa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba Wajumbe wengi walihoji juu ya utendaji wa Baraza la Manispaa. Napenda kurudia kueleza kwamba Serikali imeunda Kamati ya Wataalam ambayo imepewa jukumu la kuangalia utendaji kazi wa Baraza la Manispaa na kutoa mapendekezo juu ya hatua za kuchukuliwa kuimarisha utendaji wa Baraza hilo. Taarifa nilizonazo ni kwamba Kamati hiyo tayari imeshakamilisha taarifa yake na hivi karibuni itawasilishwa Serikalini.

KUHUSU ULINZI SHIRIKISHI:

Mhe. Spika, suala la ulinzi shirikishi ni jambo zuri na tunapaswa kuliunga mkono Jeshi la Polisi. Mpango huu utaondoa maovu mengi katika jamii na kuimarisha amani na utulivu katika nchi yetu. Hivyo, nawaomba Viongozi wote na Wananchi kwa ujumla kuongeza ushirikiano na Jeshi letu la Polisi ili tuweze kufikia lengo letu la kuanzisha na kuimarisha ulinzi shirikishi katika jamii yetu.

MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO – *CDF*:

Mhe. Spika, Baraza lako Tukufu limeidhinisha jumla ya Shilingi 540,000,000 kutumika kwa miradi ya maendeleo ya wananchi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(Consolidated Development Fund).* Vile vile, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeidhinisha jumla ya Shilingi 1,200,000,000 kutumika kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Zanzibar. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuwa na mashirikiano ya karibu kati yao na Waheshimiwa Wabunge na wananchi katika kuzitumia fedha hizo katika majimbo yao kwa miradi mbali mbali itayoibuliwa na wananchi wenyewe ili ziwe na manufaa makubwa ya maendeleo kwa wananchi hao. Fedha hizo zimetolewa na Serikali kwa ajili ya maendeleo ya Miradi ya Wananchi. Hivyo, ni vyema

zikapatikana taarifa za utekelezaji wa Miradi itakayotumia fedha hizo ikiwa ni pamoja na taarifa kamili za matumizi ya fedha hizo.

MASLAHI YA WATUMISHI WA SERIKALI

Mhe. Spika, kama ilivyokwisha kuelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ahadi ya Serikali ya kuanza kulipa mishahara mipya kwa Wafanyakazi itatekelezwa kuanzia mwezi Oktoba, 2011. Tayari Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inalifanyia kazi suala hili.

NIDHAMU NA UWAJIBIKAJI KAZINI:

Mhe. Spika, kama tunavyokumbuka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alifungua na kuendesha Semina Elekezi kwa Waheshimiwa Viongozi na Watendaji wa Serikali kwa lengo la kutoa maelekezo ya kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika shughuli za Serikali. Aidha, Semina hizi zilikuwa na nia ya kuwataka Viongozi na Watendaji kubadilika katika kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma kwa Wananchi. Ni imani yangu kwamba kufuatia mafunzo hayo, utendaji wetu utabadilika na kuwa utendaji wenye kujali maslahi ya wananchi badala ya kuweka mbele maslahi yetu binafsi. Nafasi tulizopewa ni kwa ajili ya kuwatumikia wananchi bila kinyongo au dharau tena kwa wakati.

SAFARI ZA NJE:

Mhe. Spika, katika kuendesha serikali yetu kwa uwazi *(transparency)* napenda kuchukua fursa hii kuelezea japo kwa uchache matunda ya safari mbili za nje za kikazi nilizozifanya kabla ya kikao hiki cha bajeti. Safari yangu ya kwanza nilimuwakilisha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein katika Visiwa vya Shelisheli (*Seychelles*). Katika safari hiyo nilionana na kufanya mazungumzo na Viongozi mbali mbali kuhusu uwekezaji Zanzibar. Kwa hivyo, nilifanikiwa kufanya mambo yafuatayo:-

> Kuendeleza ushirikiano katika nyanja za uchumi kwa kuziingiza sekta muhimu kama utalii na uwekezaji viwanda vidogo vidogo, pamoja na kuzingatia suala la uharamia katika kuimarisha biashara baina ya nchi za ukanda wetu wa Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, kwa hivyo, malengo hayo yalianza kwa matayarisho yake ya mara moja kwa kutembelea viwanda vya Samaki vya *Ocean Tuner Fisheries* na *Oceana Fisheries* kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Taasisi hizo kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kuja kuwekeza hapa Zanzibar. Hali hiyo pia imeleta matumaini kwa

uongozi wa Kiwanda cha *Ocean*akuonesha nia ya kuja kuwekeza na hivi karibuni ujumbe wa wawekezaji hao ulifika Zanzibar kwa ufuatiliaji wa suala hilo.

Safari yangu ya pili, Mhe. Spika, nilikwenda Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ambako nilikutana na kuzungumza na Mhe. Dkt. Mahmoud Ahmed Nejad, Rais wa nchi hiyo. Mbali na kuwakumbusha makubaliano yaliyokwisha fanywa baina ya Iran na Tanzania na suala la misaada kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tulikubaliana kuunda Tume ya Wataalamu wa Serikali ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kutathmini makubaliano yetu na kuona kilichochelewesha utekelezaji wake.

Aidha, katika mazungumzo yetu tuliomba fursa za masomo kwa Madaktari wa Zanzibar na tulikubaliwa. Pia niliahidiwa kupewa US$1,800,000 kwa ajili ya ununuzi wa *Power Tiller, Fibre Boat,* uimarishaji wa Chuo cha Utalii na ufugaji wa nyuki na mafunzo yake. Tayari fedha hizo zimekwisha idhinishwa na miradi hiyo karibu itaanza.

Mhe. Spika, katika mijadala ya Waheshimiwa Wajumbe ilionekana ipo haja ya kupata vyanzo vya umeme mbadala badala ya kutegemea chanzo kimoja. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kutafuta wawekezaji ambao watakuwa tayari kuja kuwekeza katika miradi hiyo. Wapo Wawekezaji ambao tayari wamekwishajitokeza kutaka kuanzisha miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia Upepo, Jua na hata kwa kutumia malighafi ya mianzi, lakini miradi hii yote Serikali bado inaendelea kuichunguza na ile tutakayoiona inafaa inakaribishwa kuekeza katika sekta hiyo.

MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, tunakabiliwa na mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ambapo Waislamu sote tutaingia katika Ibada ya Mfungo wa Ramadhan. Nachukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie funga njema na baraka katika nchi yetu. Aidha, nawaomba wananchi na hasa wafanyabiashara wa vyakula, nguo na mahitaji mengine muhimu walete nchini bidhaa zenye viwango bora na kuuza kwa bei nafuu. Ni vyema kama ilivyo kawaida yetu tuzidi kufanyiana wema katika mwezi huu na kuacha yote yaliyokatazwa ili kupata Baraka za Mwenyezi Mungu na kheri katika nchi yetu. Nawapongeza na kuwashukuru kwa namna ya kipekee wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo kwa kuendelea kuagiza bidhaa muhimu na kuweza kutosheleza mahitaji ya chakula na bidhaa nyingine hapa nchini. Nawatakia Wananchi wote saumu njema.

SHUKRANI:

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo yangu hayo mafupi sina budi kwa mara nyengine tena kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa mshikamano waliouonesha kwa kipindi chote tulichokuwa tukijadili na kupitisha Bajeti ya mwaka 2011/2012 na Miswada ya Sheria iliyowasilishwa. Aidha, nawashukuru Washirika wetu wa Maendeleo kwa jinsi wanavyoendelea kutuunga mkono katika mipango yetu ya maendeleo. Pia nawashukuru wananchi wa Zanzibar kwa namna wanavyoiamini Serikali yao na kujenga matumaini makubwa ya maendeleo ya nchi yetu. Tunawaahidi kuwa kazi hiyo tutaifanya kwa dhati na kwa uwezo wetu wote. Mhe. Spika, napenda kuzishukuru Kamati za Kudumu kwa kazi nzuri waliyofanya kupitia bajeti zetu na hatimae kutoa maoni muafaka ambayo yamesaidia katika kuzipitisha bajeti hizo.

Mhe. Spika, mwisho, nawatakia Waheshimiwa Wajumbe wote safari njema nay a salama ya kurudi majimboni mwao kuwatumikia wapiga kura wao.

HITIMISHO:

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kuliahirisha Baraza lako Tukufu hadi tarehe 12 Oktoba, 2011 saa 3.00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba hii ambayo ina maelekezo mengi, nasaha nyingi hasa kuhusiana na shughuli zetu za baraza, lakini pia nakushukuru kwa kuwatakia WAheshimiwa Wajumbe na wananchi wote saumu njema ambayo inatukabili si muda mkubwa kuanzia leo. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na sasa basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuahirisha mkutano huu kuna matangazo manne. Tangazo la kwanza tunawakumbusha Waheshimiwa Wajumbe kwa ile semina ambayo tumealikwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora itakuwepo kama ilivyoahirishwa kabla, kesho tarehe 01/08/2011 saa 2:30 asubuhi katika Hoteli ya Zanzibar Ocean View tunaarifiwa sote tusikose semina hiyo muhimu inayohusu masuala ya kudhibiti rushwa pamoja na masuala mbali mbali ya maadili.

Waheshimiwa Wajumbe tangazo la pili, ni kwamba tunaarifiwa ile safari ya kwenda Tunguu nadhani kuna mambo mambo huko basi itakuwepo leo Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wanahusika bila ya shaka wanajijua, mara baada ya kuahirisha kikao hiki.

Tangazo la tatu Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba baada ya shughuli zetu za kuahirisha kikao hiki Waheshimiwa Wawakilishi wa CCM wanawake wanaarifiwa kwamba kutakuwa na uchaguzi wa kuwachagua viongozi wao. Na tangazo la nne na la mwisho Meneja wa timu yetu kabambe kabisa ya Baraza la Wawakilishi ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe sote pamoja na wafanyakazi kwamba yale mazoezi tunayofanya kila siku asubuhi yatakuwa yanaendelea kuanzia tarehe 03/08/2011 saa 12:00 asubuhi katika uwanja wa Mao-Tse-Tung, mnaombwa Waheshimiwa Wajumbe tushiriki kwenye mazoezi hayo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo na mimi nawatakia saumu njema na turudi majumbani kwetu salama usalimini. Baada ya hayo basi sasa naahirisha kikao hiki hadi siku ya tarehe 12/10/2011 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 3:45 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi tarehe 12/10/2011 saa 3:00 asubuhi)